



# Mzozo wa Nyumbani na wa Kifamilia katika Jamii za LGBTIQ

## Nchini Australia, mzozo wa nyumbani na wa kifamilia haukubaliwi.

Watu wanaotambuliwa kama Wasagaji, Basha, Wanaovutiwa na Jinsia Zote, Waliobadilisha Jinsia, Wenye Jinsia Zote na Wasiokuwa wa Kawaida (Lesbian, Gay, Bisexual, Transgender, Intersex and Queer (LGBTIQ) wana haki sawa nchini Australia, na ubaguzi wote ni kinyume cha sheria.

Nchini Australia, mahusiano yote ni sawa chini ya sheria. Hii inamaanisha kwamba wapenzi wote, ikiwa ni pamoja na wapenzi wenye jinsia moja, wana haki ya kuwa katika uhusiano au kufunga ndoa.

Kila mtu ana haki ya kuwa katika mahusiano mazuri na salama na familia, marafiki na wapendwa wao.

Mzozo wa nyumbani na wa kifamilia ni uhalifu na ni kinyume cha sheria. Mtu anayetekeleza uhalifu huu anaweza kufungwa jela, awe ni mwanamume au mwanamke.

Ikiwa wewe au mtu unayemjua yuko hatarini, piga simu kwa polisi, nambari ya simu **000**.

Polisi nchini Australia ni salama na wanaweza kuaminika.

Kwa ushauri na maelezo ya bila malipo na ya siri, piga simu kwa 1800RESPECT, nambari ya simu **1800 737 732**.

Ikiwa unahitaji mkalimani bila malipo piga simu kwa **131 450**.

## Serikali ya Australia (Australian Government) haikubali mzozo wa nyumbani na wa kifamilia chini ya hali yoyote ile.

Mzozo wa nyumbani na wa kifamilia hujumuisha tabia au vitisho ambavyo vinalenga kudhibiti mwenzi kwa kusababisha hofu au kutishia usalama wao. Mzozo wa nyumbani na wa kifamilia unaweza kujumuisha:

- kupiga;
- kunyonga;
- kunyima fedha muhimu kwa mpenzi au familia;
- kumtenga mpenzi kutoka kwa marafiki na familia;
- matusi au kukosoa mpenzi; na
- kuwatishia watoto au wanyama-vipenzi.

Mzozo wa nyumbani na wa kifamilia katika mahusiano ya LGBTIQ unaweza pia kujumuisha:

- kutishia kutumia hali ya mwenzi kuwa na jinsia mbili, ujinsia, jinsia, hali ya kijinsia, hali ya kubadilisha jinsia au ya HIV dhidi yao;
- kutishia 'kufichua' mwenzi kwa familia, marafiki, jamii au mahali pa kazi'
- kudhibiti dawa za mwenzi au ufikiaji wa huduma ya afya inayohusiana na kubadilisha jinsia; au
- Kumshinikiza mwenzi kukubali kanuni za ngono au jinsia.

## Kuna huduma za usaidizi nchini Australia ambazo zinaweza kukusaidia.

ACON hutoa maelezo bila malipo kuhusu masuala ya kiafya yanayoathiri watu wa LGBTIQ, ikiwa ni pamoja na mzozo wa nyumbani na wa kifamilia. Nenda kwenye tovuti ya **ACON** kwenye [www.acon.org.au](http://www.acon.org.au) ili kupata orodha ya huduma jumuishi za usaidizi za LGBTIQ.

**1800RESPECT** ni huduma ya ushauri wa mzozo wa kijinsia, uhasama wa kifamilia na kinyumbani kutoka kwa taifa la Australia (Australia's national sexual assault, family and domestic violence counselling service). Hutoa maelezo na ushauri wa mtandaoni na wa simu bila malipo na wa siri. Washauri watakusikiliza, watajibu maswali na kukuelekeza kwa huduma nyingine za msaada katika eneo lako.

Piga simu kwa **1800 737 732** au nenda kwenye sehemu ya maelezo maalum ya LGBTIQ kwenye tovuti ya **1800RESPECT** kwenye [www.1800RESPECT.org.au](http://www.1800RESPECT.org.au).

## Je, unahitaji mkalimani?

Piga simu kwa **Huduma ya Ufasiri na Ukalimani (Translating and Interpreting Service (TIS))**, nambari ya simu **131 450**. Mkalimani kutoka TIS anaweza kukusaidia kuwasiliana na huduma zingine, hata hivyo TIS haitoi huduma ya ushauri. Simu zote hazilipishwi na ni za siri.